

SWALI: Maana yake ni nini Bwana anaposema (Mathayo 19)

“Maana wako 1.MATOWASHI-waliozaliwa hali hiyo toka
MATUMBONI MWA MAMA ZAO; Tena wako

2.MATOWASHI-waliofanywa na WATU kuwa matowashi; tena wako

3.MATOWASHI-WALIOJIFANYA KUWA MATOWASHI KWAAJILI YA
UFALME WA MBINGUNI.Awezaye kulipokea neno hili,na alipokee”.

JIBU: Matowashi ni watu waliojitoa wakfu kwa Mungu,
wasiojikusisha na mambo ya wanawake,(yaani kuwa na mke au
watoto), mfano wa matowashi katika biblia ni Bwana wetu Yesu,
Mtume Paulo,Barnaba, n huwenda pia Yohana mbatizaji, Danieli
na Eliya Mtishbi.

Sasa wapo wa aina tatu, wapo ambao tangu kuzaliwa tumboni
mwa mama zao Mungu aliwaumba hivyo, hawana uwezo wa
kuzalisha, wengi miongoni mwa hao Mungu amewachagua wawe
wakfu kwake...kwa ajili ya utumishi wake.

Kadhalika wapo wengine wamehasiwa, hao ndio waliofanywa na watu kuwa hivyo kwa ajili ya ufalme wa mbinguni...

Na pia wapo ambao wameamua kujifanya wenyewe kuwa matowashi..hawa hawajahasiwa wala hawana shida yoyote isipokuwa wao wenyewe wameamua kubaki hivyo hivyo wasioe kwa ajili ya ufalme wa mbinguni yaani wajishughulisha na mambo ya ufalme wa mbinguni kwa uhuru zaidi..mfano wa hao ni Bwana wetu Yesu, Mtume Paulo, Barnaba.

Na kama Bwana Yesu alivyosema mtu yoyote awezaye kulipokea neno hilo na alipokee alikuwa anamaanisha kwamba “mtu akitaka kuwa hivyo na awe” ila sio lazima kama kama Mtume Paulo pia alivyosema kwa uweza wa Roho katika *1 Wakorintho 7:26-40*.

Na pia kumbuka hiyo ni KARAMA watu wa namna hiyo huwa wanaona mke/mume kwao si kitu cha thamani kubwa sana kama kuwa tu karibu na Mungu. Hawajilazimishi wala kutumia nguvu nyingi kufanya hivyo, tofuati na wengi wanavyodhani. Mwanamke aliyejitoa kwa Mungu, kaamua kutojishughulisha na mambo ya mume, huyo naye anatafsirika kama towashi.

Ubarikiwe.

Ikiwa utahitaji msaada zaidi ya mafundisho ya kila siku/maombezi/ubatizo/ushauri basi wasiliana nasi kwa namba zetu hizi +255693036618/+2557890001312

Au jiunge na makundi yetu ya mafundisho ya kila siku kwa kwa njia ya Whatsapp kwa kubofya hapa >>>> WHATSAPP GROUP

Mada zinaendana:

JE NI HALALI KUOA WAKE WENGI, AU KUTOA TALAKA?

JE! NI SAHIHI KWA MKRISTO KUOA/KUOLEWA NA MTU WA IMANI NYINGINE?

BIBLIA INASEMA ASKOFU ANAPASWA AWE MUME WA MKE MMOJA!
JE! WALE WASIOOA KWA AJILI YA INJILI HAWAWEZI KUWA MAASKOFU?

NAFASI YA MWANAMKE KATIKA KANISA

Matowashi ni wakina nani?

Rudi Nyumbani:

Share on:
WhatsApp

Print this post